

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA**

Shule ya Sekondari Chinongwe

SLP 27

Ruangwa

12 Desemba 2019

KUMB.NA.CHSS/EE.10/24

Jina la Mwanafunzi.....

Shule Atokayo.....

Anuani.....

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI YA KUTWA YA  
CHINONGWE MWAKA 2021**

1.Ninayo furaha kukuharifu umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule hiiipo katika kata ya Chinongwe, Tarafa ya Mnacho ,Wilaya ya Ruangwa.Shule hii ipo km 63 kutoka makao makuu ya wilaya

**DIRA YA SHULE**

Dira ya shule yetu ni kumkuza mwanafunzi kiakili,kiroho na kimaadili ili aweze kuihudumia jamii yake.

**KAULI MBIU YA SHULE(SCHOOL MOTTO)**

Elimu haina mwisho

**MAWASILIANO**

Lugha itumikayo kuwasiliana baina ya wanafunzi na walimu au wanafunzi kwa wanafunzi ni kingereza

**2.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2:1 SARE ZA SHULE**

**(A)WAVULANA:**

i.Suruali mbili(2)rangi ya damu ya mzee mapana nane (8) na shati mbili nyeupe(hakikisha unanunua kama hivyo ulivyoagizwa)

Yii.Viatu pea mbili vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu

- iii.Soksi nyeupe jozi mbili
- iv. T-Shirt za shule rangi ya blue yenye Kora(form six)
- v.Tai ya rangi ya damu ya mzee
- vi.Trak suit ya rangi ya bluu/nyekundu kwa ajiri ya michezo

#### **(B)WASICHANA.**

- i.Sketi mbili za kuvuka magoti za rangi ya damu ya mzee(nzito)
- ii.Shati nyeupe mbili
- iii.Soksi nyeupe jozi mbili
- iv.T-shirt rangi ya blue yenye Kora(form six)
- v.Viatu jozi mbili vyakufunga kamba visivyo na kisigino kirefu
- vi.Hijabu inaruhusiwa ya rangi nyeupe(au Nusu kanzu kwa wasichana bluu kwa ajiri ya kuva siku anazovaa T-shirt)
- viii. Track suit ya michezo rangi ya bluu/nyekundu

N.B:Wasichana wote wanaokaa mbalina shule wanatakiwa wakae Bwenini.Wazazi mnatakiwa kufika shulen i kwa ajiri ya kupatiwa maelekezo ya utaratibu wa kukaa bwenini.

#### **2.2 VIFAA VINGINE**

- a)Daftari kubwa (counter book)kumi nambili (12) pamoja na peni na penseli
- b)Kamusi ya kingereza na Kiswahili
- c)ream moja
- d)Jembe,Mfagio na kwanja/panga.

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 Mwanfunzi anatakiwa awahi siku hiyo kwa ajili ya kuanza kozi ya Kiingereza.

Mwisho wa kuripoti mwanafunzi ni tarehe 18Januari 2021

Ahsante.

RAMADHANI K MAYENGO

MKUU WA SHULE

SIMU 0789269778